



Ndovu na vyura

Mozambican folktale
Kiswahili




Hapo kale, mfalme wa
mwitu alikuwa Bw.
Simba.




Aliwatuma wanyama
wake kukomesha kelele
zilizotoka kwenye ziwa
ndogo mwituni.

Lakini hawakufaulu!




Ndovu alijitolea
kukomesha.

Ndovu alitumwa nje
kuwa mlinzi.



Usiku wa manane kelele
zilianza na ndovu
akaanza kuua vyura.

Alifanya vile vile siku
iliyofuata.




Baada ya majuma kadhaa, Mfalme Simba alikuwa mwenye furaha kwa kuwa ndovu alikomesha kelele.



Lakini baada ya mwezi,
waliona wadudu
shambani mwao.




Mfalme Simba
alimuuliza ndovu
kuwaita vyura waende
kuwala wadudu.



Ndovu alijawa na uoga
kwa vile alikuwa
amewaua wote.

Alisema: Samahani,
samahani, ni-li-waua
wote!




Kisha Mfalme Simba
alisema: Ndovu,
nilikuuliza kukomesha
kelele, siyo kuua vyura.

Ndovu aliwekwa
gerezani miaka mingi!



Mfalme aliwaambia
wanyama wote wafanye
kila alilosema wakati
wote.




Ndovu na vyura

Writer: Mozambican folktale

Illustration: Amir Bachir António Necas

Translated By: Caren Echesa

Language: Kiswahili



Hadithi hii iliandikwa mwaka wa 2013 na wanafunzi wa Universidade Pedagogica-Maxixe, Musumbiji kutoka kwa fikra zao baada ya kusimuliwa nyumbani na kuboreshwa na mwalimu wao wa Kiingereza, Ingrid Schechter.

© Mozambican Writers



This work is licensed under a Creative Commons Attribution (CC-BY) Version 3.0 Unported Licence

Disclaimer: You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute or credit the original author/s and illustrator/s.

Saide
South African Institute
for Distance Education

www.africanstorybook.org
A Saide Initiative